



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI**



[Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Kigamboni]

Simu: +255 22-2928468
Fax: +255 22-2928469
Baruapepe: info@kigambonimc.go.tz
Tovuti: www.kigamboni.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:

S.L.P. 36009,
KIGAMBONI,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

Kumb. Na. VA.9.386/01/102

Tarehe 06/07/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imepokea kibali cha kutekeleza Ikama na Bajeti kuhusu Ajira mpya katika mwaka wa fedha **2021/2022** chenye Kumb. Na. **97/228/01/9** cha tarehe **13 Mei, 2022** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni anawatangazia Wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi zilizoorodheshwa hapo chini:-

1. DEREVA DARAJA LA II - (NAFASI 7)

(i) Sifa za mwombaji:-

Kuajiriwa mwenye cheti cha kidato cha nne (Form IV) na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

(ii) Majukumu ya kazi:

- (a) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- (b) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- (c) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- (d) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- (e) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- (f) Kufanya usafi wa gari, na
- (g) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

Kwa kuzingatia Ngazi ya mshahara ya Serikali yaan TGS B₁ kwa mwezi